

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO TARATIBU ZA USAJILI WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI (KWA MUJIBU WA SHERIA YA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI NA. 24, 2002)

### 1.0 TARATIBU ZA USAJILI

Usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unaofanyika chini ya sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Na. 24 ya mwaka 2002 umegawanywa katika ngazi nne kama ifuatavyo:

- 1.1 Ngazi ya Wilaya
- 1.2 Ngazi ya Mkoa
- 1.3 Ngazi ya Taifa
- 1.4 Ngazi ya Kimataifa

Mhajili wa Mashirika ya kiserikali amepewa mamlaka chini ya kifungu cha 22(1) cha sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24, ya mwaka 2002 kuteua maafisa wa umma katika wilaya au mkoa kwa ajili ya kuwezesha usajili katika ngazi husika. Katika mfumo uliopo sasa maafisa wa umma wanaotajwa katika sheria ni Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya na Mkoa ambao kwa namna nyingine huitwa wasajili wasaidizi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 12(1) cha sheria, maombi ya usajili yatawasilishwa na kikundi cha watu kwa Msajili kupitia fomu maalumu (NGO A Fomu Na. 1). Maneno %kikundi cha watu+ yanahusisha kikundi cha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Hata hivyo, kanuni ya 3 ya kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zilizofanyiwa marekebisho mwaka 2015 kupitia tangazo la serikali Na. 8 inaweka sharti la kikundi kuwa na watu/wanachama wasiopungua watano.

**Kulingana na Kifungu cha 12(2) cha Sheria ya NGOs Na. 24/2002, Maombi ya usajili wa NGOs yanatakiwa kuwa na viambatanisho vifuatavyo:-**

- a) Katiba ya Shirika lisilo la Kiserikali (Nakala 3 zilizojaladiwa - Bound).
- b) Maelezo binafsi (Wasifu) wa viongozi 3 (CV) na picha 2 kwa kila CV - (Mwenyekiti, Katibu na Mhazini, au wengineo kulingana na mahitaji ya Shirika)  
**Angalizo: kwa NGOs za Kimataifa - CV mbili ziwe za raia wa Tanzania.**
- c) Muhtasari wa kikao cha kuanzishwa kwa Shirika ukiambatanishwa na majina na saina za wanachama waanzilishi.
- d) Fomu ya maombi ya usajili (**NGO A Fomu No. 1**) iliyojazwa na mwombaji/waombaji na kubandikwa ushuru wa stempu za shilingi **1,500/= au Dola za Kimarekani 2** kwa NGOs za Kimataifa.
- e) Barua ya Utambulisho kutoka kwa Msajili Msaidizi (Afisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa, Halmashauri /Manispaa/Wilaya).
- f) Maelezo yoyote au taarifa kama itakavyohitajiwa na Msajili.

**2.0 ADA ZA USAJILI**

- a) Ngazi ya Wilaya - **Shs 80,000/=**
- b) Ngazi ya Mkoa - **Shs 100,000/=**
- c) Ngazi ya Taifa - **Shs 115,000/=**
- d) Ngazi ya Kimataifa - **Dola za Kimarekani 350**

Maombi yatumwe kwa;

Msajili wa NGOs,  
Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto,  
8 Barabara ya Kivukoni  
S.L.P 3448  
**11486 DAR ES SALAAM.**

*Simu 213526/2137679/2123146*

*Tovuti -<http://www.tnnc.go.tz>*